**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

*Simu:* +255 026 2322761-5
*Fax No.* +255 026 2324218
E-mail: **cna@bunge.go.tz**

Ofisi ya Bunge,
10 Barabara ya Morogoro
S.L.P. 941,
40490 Tambukareli,
**DODOMA**

# TAARIFA KWA UMMA

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira imepanga kupokea maoni ya wadau kuhusu **Mkataba wa Uanzishwaji wa Taasisi ya Ukuzaji wa Maendeleo ya Kijani Duniani (Agreement on Establishment of the Global Green Growth Institute)** kwa mujibu wa Kanuni ya 111(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025***.***

Mkutano wa kupokea na kusikiliza maoni ya wadau (Public Hearing) utafanyika siku ya **Jumamosi tarehe 15 Agosti, 2026 kuanzia saa 6:00 mchana katika Ukumbi wa Philip Marmo**, Bungeni Jijini Dodoma.

Kwa kuzingatia umuhimu wa Mkataba huo, Kamati inawaalika wadau wote kufika kwenye Mkutano huo na kuwasilisha maoni yao kabla ya kupelekwa katika hatua nyingine.

Aidha, maoni yanaweza pia kuwasilishwa kwa njia ya posta kupitia anuani ya Ofisi ya Bunge au kupitia Barua pepe ya *cna@bunge.go.tz* na kamati@bunge.go.tz.

Mkataba huo unaweza kupakuliwa katika Tovuti ya Bunge https://www.parliament.go.tz/documents/resolutions

**Imetolewa na:** Kitengo cha Mawasiliano na Elimu kwa Umma,
Ofisi ya Bunge,
**DODOMA.**

10 Agosti, 2026.